OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

NAMBA ZA SIMU

Mkuu wa Shule: **0766072210 / 0688652722**

Makamu Mkuu wa Shule: **0713075576**

SHULE YA SEKONDARI KASELA,
S.L.P 481,
NZEGA-TABORA.

12 /12/2020

MZAZI/MLEZI WA……

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KASELA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA MKOA WA TABORA MWAKA 2021**

1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari KASELA ipo umbali wa Km 27 kutoka nzega mjini.

Muhula masomo utaanza tarehe 11/01/2021 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2020 na mwisho wakuripoti ni tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. SARE YA SHULE.

- Sare ya shule hii ni kijivu na bluu nyeusi kwa wavulana na wasichana.
- Kwa msichana anatakiwa kuwa na sketi mbili ndefu zilizo vuka magoti na mashati mawili meupe yenye mikono mifupi.
- Kwa mvulana awe na suruali mbili zisizo bana (modo) na mashati mawili meupe mikono mifupi.
- Kwa wavulana na wasichana wanatakiwa kuwa na sweta la kijivu kwa ajili ya kujikinga na baridi na tisheti ya bluu nyeusi
- Viatu vyeusi jozi mbili (2) vya ngozi vya kufunga na kamba, visiwe na sori ndefu na visivyo chongoka mbele.
- Soksi jozi mbili (2) rangi nyeusi
- Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi.
- Tai mblili yaani kijivu na bluu nyeusi.

B. SARE YA MICHEZO KWA SHULE HII

- Tisheti ya kijivu na bukta ya bluu kwa wavulana.
- Tisheti ya kijivu na track suit rangi ya bluu.

C.VIFAA VYA KUJIFUNZIA

- Daftari kubwa zisizopungua tisa.
- Kalamu za wino
- Kalamu za mkaa
- Mkebe wa hesabu
- Ruler

2.1 SHERIA NA KANUNI MUHIMIJ ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayo tolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakaz iwote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya Shule
iii. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya Shule
vii. Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

ix. Vitu kama pete, kofia nk haviruhusiwi kuvaliwa shulenl. Ukikutwa navyo utanyang'anywa na vitachomwa moto na adhabu nyingine itafuata

2.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

a) Wizi

b) Kutohuduria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro au kutofanya mazoezi na majaribio darasani.

c) Kugoma, kuhamasisha kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shue au watu

d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/ walezi na jamii kwa ujumla

e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule

f) Kufuga nywele ndefu.

g) Kufuga ndevu

h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

i) Uvutaji wa sigara

j) Uasheratj,uhusiano wa jinsi moja (ushoga)

k) Ubakaji

l) Kushiriki katika matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja Sheria za nchi

m) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana

n) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

o) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya Shule, Kabidhi simu kwa makamu mara unaporipoti shule.

p) Kudharau bendera ya Taifa

q) Kukataa adhabu kwa makusudi

r) Uharibifu wa mali ya uma kwa makusudi

2.3 VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

- Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali na kuwasilishwa kwa mkuu wa shule na mwanafunzi atakapo ripoti.
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi,na mkataba wa kutoshiriki katika migomo fujo na makosa ya jinai.
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
BENJAMIN PETER NGUNZU
MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

SHULE YA SEKONDARI KASELA

MKATABA WA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI

Unashauriwa kujaza fomu hii ya mapatano kikamilifu.

SEHEMU A: MWANAFUNZI

Mimi _____ Nimesoma na kuelewa vizuri sheria, maagizo na kanuni zote zashule. Nakubali / sikubali nafasi hii na kuwa nitatumia uwezo wangu wote kujiendeleza kitaaluma, nitatii Sheria,maagizo na kanuni zote za shule na wala sitashiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai.

SAHİHİ_____ TAREHE_____

SEHEMU B: MZAZI/MLEZI.

Mimi _____ Mzazi/Mlezi wa_____ umepokea taarifa ya mwanangu ya kujiunga na shule ya sekondari KASELA. Kwa kutambua umuhimu wa Elimu na wajibu wangu, naahidi kuwa muda wote mwanangu atakapokuwa shuleni nitashirikiana na Uongozi wa shule kumlea mtoto kwa kufuata sheria ,maagizo na kanuni zote za shule na kuhakikisha kuwa anahudhuria masomo kwa kadri ya ratiba ya shule, nitatekeleza maelekezo yote yatakayotolewa na shule.

SAHİHİ_____ TAREHE_____

MEDICAL CERTIFICATE FORM

KASELA SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 481,

NZEGA

DATE……

MEDICAL OFFICER……..

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine the above named as to His/ Her fitness as indicated below. Arrange for necessary treatment so that the certificate may be signed and brought to school by the student.

This certificate must be signed by a qualified medical officer of recognized Hospital

---

MEDICAL CERTIFICATE.

I have examined the above named student with regard to:-

Skin……Abdomen……..

Eyes……Urine……..

Teeth……Hemoglobin……

Spleen……..Chest……

Any Disabilities……

I consider that:-

He/she is in good health free from infections, and fit to come to school……..

He/she is not fit to come to school after having……..

Treatment for……

Name & Signature……. Date……

MEDICAL OFFICER